



Jiji la Makimbilio ni nini?

Katika jiji la makimbilio, wanajumuiya wote wanaweza kupata huduma za Jiji bila kuulizwa hadhi yao ya uhamiaji.

Ndani ya New Westminster, serikali ya halmashauri ina jukumu katika maeneo kama vile ukingaji wa moto, maktaba, vituo vya jumuiya, mbuga, burudani na maegesho ya magari.

Baadhi ya watu wa New Westminster wanaweza kuogopa kukamatwa na kurudishwa makwao na Wakala wa Huduma za Mipaka ya Canada (CBSA), na wanaweza wasitumie huduma za Jiji iwapo mtu atawauliza kuhusu hadhi zao za uhamiaji. Sera ya Jiji la Makimbilio inasema kuwa kila mmoja anakaribishwa kushiriki katika kila kitu kinachotolewa na jiji la New Westminster bila kuulizwa na mfanyakazi wa Jiji kuhusu hadhi ya uhamiaji.




NEW WESTMINSTER

JIFUNZE ZAIDI

Kama ukitaka kujifunza zaidi kuhusu Sera ya Jiji la Makimbilio, tafadhali tembelea tovuti yetu ya newwestcity.ca/sanctuary-city

MASWALI?

Wasiliana nasi kupitia
plnpost@newwestcity.ca


NEW WESTMINSTER

Jiji la Makimbilio

Kuhakikisha wakazi na wegeni wote wa New West wanapata uwezo wa kuzifikia vifaa vya Jiji, programu na huduma.



Jiji la New Westminster litatekelezaje sera hii?



1 Tutawasiliana na umma kuhusu sera hii kupitia machapisho, kampeni za mitandaoni na video.



2 Tutawaelimisha na kuwafundisha wafanyakazi wa Jiji jinsi ya kuitumia sera hii katika kazi zao za kila siku.



3 Wafanyakazi wa Jiji wanafundishwa chini ya Mfumo wa Utofautishaji, Usawa, Ujumuishaji na Upinga-Ubaguzi. Mfumo huu unaunga mkono sera ya Jiji la Makimbilio. Mfumo huu vile vile unatoa muongozo katika ufundishaji wa wafanyakazi harakati za kupinga ubaguzi zinazoendelea na za usoni.



4 Kituo cha Makaribisho katika shule ya upili ya New Westminster ni mahali muhimu kwa maelezo kuhusu sera na mahala pa katikati kuingia kwenye Jiji.



Kwenye bwawa la kuogelea

Sera hii inatumika kwenye vifaa, programu, na huduma zinazotolewa na Jiji la Westminster. Haitumiki moja kwa moja na Idara ya Polisi ya Westminster.

Wanatayarisha sera yao sambamba na hii.

Sera ya Jiji la Makimbilio ni sehemu muhimu ya ahadi ya Jiji ya kutengeneza jamii jumuisho iliyo bora zaidi.



Jiunge na darasa la kufanya mazoezi ya mwili



Inatumika kwa nani?

Kanda yetu ni nyumbani kwa wahamiaji na wakimbizi wengi. Hii ndivyo ilivyo kwa New Westminster vile vile. Baadhi ya watu ni wahamiaji ambao hawakuandikishwa.

Kuna sababu kadhaa kwa nini watu hawakundikishwa. Vibali vya kazi kwa wafanyakazi wa muda mfupi kutoka nje vinaweza kuwa vimeisha muda wake. Uvunjikaji wa ndoa unaweza kumuacha mtu bila kuwa na udhamini. Wanafunzi wanaweza kuzidisha muda wao wa masomo au vibali vya kazi. Watu wanaweza kupoteza hadhi zao au madai yao ya ukimbizi kukataliwa. Baadhi ya watu wanaweza kuwa ni wahanga wa biashara haramu ya kusafirisha watu. Hizi ni mifano ya sababu chache ya kile kinachoweza kutokea.



Fanya tathimini



Je inanigusaje?

Sera haiwagusi wakazi wa New Westminster wenye hadhi za uhamiaji zinazotambulika. Sera hii kwa uchache, inamaanisha kuwa kila mmoja, bila kujali hadhi zao za uhamiaji, wanaweza kutumia vifaa vya Jiji, programu na huduma bila mfanyakazi wa Jiji kuuliza kuhusu hadhi zao.

Ada na michakato inatumika kwa waombaji wote. Hakuna msaada wa kifedha kwenye sera hii. Wakazi wote wanaweza kutuma maombia ya msaada wa kifedha kwenda Programu ya Msaada wa Fedha wa Mbuga & Burudani na hawataulizwa hadhi ya uhamiaji. Jiji limewania kupunguza vikwazo katika ushiriki.

Jifunze Zaidi: Kama ukitaka kujifunza zaidi kuhusu Sera ya Jiji la Makimbilio, tafadhali tembelea tovuti yetu ya newwestcity.ca/sanctuary-city

Maswali? Wasiliana nasi kupitia plnpost@newwestcity.ca